

# Kile cha Kutarajia: Nakala kuhusu Kutembelea Kliniki ya Chanjo Inayohamishwa Kutoka Sehemu Moja Hadi Nyingine

Kliniki za chanjo zinazohamishwa kutoka sehemu moja hadi nyingine hukuletea chanjo ya COVID-19 ulipo na kwa jamii yako. Video hii inakuonyesha hatua kwa hatua kile unaweza kutarajia unapotembelea kliniki ya chanjo inayohamishwa kutoka sehemu moja hadi nyingine.

Unapofika kwenye kliniki inayohamishwa kutoka sehemu moja hadi nyingine utaandikishwa na mtu anayekusalimia kwa ajili ya miadi yako ya chanjo.

*[Mtu Anayekusalimia] Hujambo! Sawa, nitahakikisha umeandikishwa leo. Jina lako la mwisho ni nani?*

Tafadhalii wajulishe ikiwa unahitaji msaada wa ufikiaji au wa lugha. Kliniki ya chanjo inayohamishwa kutoka sehemu moja hadi nyingine mara nyingi huwa na fursa za wanaokuja bila miadi, kwa hivyo mlete rafiki!

*[Mtu Anayekusalimia] Wewe umeshaandikishwa, unaweza kuelekea kwenye foleni.*

Subiri zamu yako moja kwa moja nje ya basi au katika eneo la kusubiri kwenye basi.

Wakati ni zamu yako ya kupata chanjo, kaa chini kwenye kituo cha chanjo pamoja na daktari. Kuna skrini zinazopatikana ikiwa ungependa faragha zaidi.

*[Daktari] Hebu niambie jina lako?*

Daktari atapitia maelezo yako pamoja na wewe na unaweza kuuliza maswali yoyote unayoweza kuwa nayo kuhusiana na chanjo.

Daktari atahitaji kufikia sehemu ya juu ya mkono wako ili akudunge chanjo.

Mara tu unapopewa chanjo, utaondoka kwenye basi.

*[Mfanyakazi] Hujambo. Asante sana kwa kuja. Asante kwa kupata chanjo. Na sasa tungependa usubiri kwa dakika 15 hivi hapa katika eneo hili.*

Utakaa katika eneo la uchunguzi kwa dakika 15. Na mfanyakazi ataelezea kile cha kufanya ikiwa hujihisi vizuri.

Wafanyakazi waliofunzwa kama wauguzi au mafundi wa matibabu ya dharura wako kwenye eneo ikiwa hujihisi vizuri.

Baada ya dakika 15 kuisha, umemaliziwa!

Asante kwa kupata chanjo.

Ikiwa una maswali kuhusu chanjo ya COVID-19, zungumza na mtoa huduma wako wa afya au tembelea tovuti yetu.

<https://www.health.state.mn.us/diseases/coronavirus/vaccine/index.html>

Minnesota Department of Health  
Communications Office  
PO Box 64975  
St. Paul, MN 55164-0975  
651-201-4989  
[health.communications@state.mn.us](mailto:health.communications@state.mn.us)  
[www.health.state.mn.us](http://www.health.state.mn.us)